# YALIYOMO.

**UTANGULIZI**.

1. **NIFANYE NINI NIOKOLEWE?**

   Sehemu Ya A
   - Kwa nini nizaliwe mara ya pili
   - Yamaanisha nini kuzaliwa mara ya pili?
   - Ni nini kinafanyika tunapozaliwa mara ya pili?
   - Ninawezaje kuzaliwa mara ya pili?
   - Ninini kitatendeka baadaye?

   Sehemu Ya B
   - Ubatizo unafuata kuamini na kutubu.
   - Ufahamu wa ubatizo wa maji.
   - Kanisa linaenea.

2. **NINAMUELEKEZAJE MTU WINGINE KWA KRISTO?**
   - Uhakika wa wokuvu wangu.
   - Hatua za kumuelekeza Mtu mwingine kwa Kristo

3. **YESU-MTUMISHI WA MUNGU.**
   - Kutimiza unabii
   - Yesu anafunza kuhusu ukuu.
   - Yesu mfano kwetu.

4. **KUTUMIKA KAMA KUHANI WA MUNGU.**
   - Nimtumikie nani?
   - Nitatumika aje?
   - Kutumika kama kuhani.

5. **KUTUMIKIA MWILI WA KRISTO NA VIPAWA VYA ROHO.**
   - Vipawa vya Roho Mtakatifu.
   - Vipawa vya Bwana aliyefufuka.
   - Vipawa vya Mungu Baba.
   - Kila anayemwamini anahududumu.
   - Tabia za mtumishi.

6. **MTUMISHI ANAYEOMBA**.
   - Kwanini tuombe?
   - Kuwaombea watakatifu.
   - Kuwaombea wale wanaohubiri na kufunza neno.
   - Kuwaombea watu wote.
   - Nini kinachotendeka kwa maombi ya watakatifu?

# UTANGULIZI.

***"Nawaandikia nyinyi watoto wandogo, kwa sababu mmesamehewa dhabi zenu, kwa ajili ya jina lake."* 1 Yohana2:12.**
***"Nawandikia nyinyi watoto wadogo, kwa sababu mmemjua Baba."* 1 Yohana 2:13.**

**Waamini wapya wanajua mambo mawili:**

- Yesu kristo amewasamehe dhabi zao.
- Sasa hao niwa jamii ya Mungu, na yeye ni Baba yao wa mbiguni.

Mafunzo haya ni ya kutupatia ufahamu kamili yamaana ya kufanyika wana wa Mungu-kuzaliwa katika jamii ya Mungu inayoitwa kanisa.
Tunapokua katika jamii hii tunatabua kuwa tunaua jibikaji kwa Mungu kwa watu wengine katika jamii hii-ndiposa kichwa "kuzaliwa mara ya pili tutumike"

***"Nina waandikia nyinyi vijana, kwa sababu mmemshinda yule muovu"* 1 Yohana 2:13b.**
***"Nimewaandikia nyinyi vijana kwa sababu mna nguvu, na neno la Mungu linakaa ndani yenu, nanyi mmemshinda Yule muovu"* 1 Yohana 2:14b**

Kwa kusoma neno la Mungu na kuachilia mapenzi ya Mungu yatushike, Tunakua ka ma vija na- Tukijengeka katika imani neno la Bwana likidumu ndani yetu, na hivyo kumshinda yule muovu.

***"Nawaandikia nyinyi, akina Baba, kwa sabubu mmemjua yeye aliye tangu mwazo."* 1 Yohana 2:13a.**
***"Nimewaandikia nyinyi akina Baba, kwa sababu mmemjua yeye aliye tangu mwanzo."* 1 Yohana 2:14a.**

Hili ndilo lengo letu: kumjua yeye tangia mwanzo, na tuwe kama akina Baba, kufunza na kuelekeza, na kuwalea waumini wapya kwa jamii ya Mungu, kuwawezesha kukua na kutumikia familia hii.
Mtume Paulo anaandika ***"ili nimjue yeye na uwezo wa kufufuka kwake, na ushirika wa mateso yake, nikifananishwa na kufa kwake; ili nipate kwa njia yoyote kufikia kiama ya wafu."* Wafilipi 3:10-11**.

Naomba kwamba mnapo soma maandishi haya, mtavutwa kumtumikia Mungu, Ndugu na dada ndani ya yesu kwa upendo ule aliokuwa nao Yesu kwetu.

***"Ee Bwana, unijulishe njia zako, unifundishe mapito yako, uniongoze katika ukweli wako na unifundishe. Maana wewe ndiwe Mungu wa wokovu wangu, nakungoja Wewe mchana kutwa"* Zaburi 25:4-5.**

Sura Ya Kwanza

# NIFANYE NINI NIZALIWE MARA YA PILI?

### SEHEMU YA [A]

**Nifanye nini niokolewe?**
Palikuwa na mtu mmoja wa mafarisayo, jina lake Nikodemo mkuu wa wayahudi huyu alimjia Yesu usiku, akamuambia, “Rabii twajua yakuwa wewe umwalimu, umetoka kwa Mungu; kwa maanahakuna mtu awezaye kuzifanya ishara hizi uzifanyazo wewe isipokuwa Mungu yu naye.”

Yesu akajibu akamwambia**, “Amin, amin** nakuambia mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme Mungu”.
Nikodemo akamwambia, awezaje mtu kuzaliwa akiwa mzee? aweza kuingia tumboni mwa mamaye mara ya pili akazaliwa?

Yesu akajibu “**Amini, amin** nakuambia, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuingia ufalme wa Mungu.Kilicho zaliwa na Roho ni roho. usistaajabu kwa kuwa nilikuambia, hamna budi kuzaliwa mara ya pili. Upepo huvuma upendako,na sauti yake waisikia,lakini hujui unakotoka wala unakokwenda; kadhalika na hali yake kila mtu aliyezaliwa kwa Roho. Nikodemo akajibu, akamwambia, yawezaje kuwa mambo haya?” Yohana 3:1-9

**KWANINI LAZIMA NIZALIWE MARA YA PILI?**

Yesu anasema tusipozaliwa mara ya pili:

Hawezi kuuona ufalme wa Mungu. Aya 3

Hawezi kuingia ufalme wa Mungu. Aya 5

**INAMAANISHA NINI KUZALIWA MARA YA PILI?**
Kielezo “kuzaliwa mara ya pili” yamaanisha kuzaliwa kutoka mbinguni. Yesu alitofautisha kati ya:

| KUZALIWA ASILI | NA | KUZALIWAKWA ROHO. |
|---|---|---|
| Kilicho zaliwa na mwili kwa ni mwili. Yohana 3:6. | . | Kilicho zaliwa kwa Roho ni roho. Yohana 3:6 |

Mtume yohana anatuambia.

> Bali wale wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminiojina lake. Yohana1:12.

Masharti ya haki hii ya kufanyika mototo wa Mungu ni kupokea Yesu kwa Roho wake ndani ya mioyo yetu. katika musingi wa kuamini, tunaweza kupokea Yesukuzaliwa mara ya pili.

Yohana1:13 - Tunazaliwa.


- **Sio kwa damu**
- **Wala kwa mapenzi ya mwili**
- **Wala kwa mapenzi ya mtu**
- **Bali kwa mapenzi ya Mungu**

Hivyo ni, tunazaliwa kutoka mbinguni ama mara ya pili.

**NI NINI KINATENDEKA NINAPOZALIWA MARA YA PILI.**

Mara tuninapo "zaliwa mara ya pili" Hivyo ni "**kuzaliwa kutoka mbinguni"** nina -

- **Alituokoa katika nguvu za giza**, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa mwana wa pendo lake. **Wakolosai 1:13.**




- **Sio mimi ninaishi -** Nilifanywa kiumbe kipya. **Wagaratia 2:20**

Kwa kuwa Kristo anadumu ndani YANGU.

- **Sitendi dhambi kwa sababu**.

> Sitendi dhambi, kwa sababu nimezaliwa kutoka mbinguni
> 1 Yohana 3:9

> Uzao wake wakaa ndani yangu
> 1Yohana 3:9.

Ninajirinda na Yule muovuhawezi kunigusa.

Twajua ya kuwa mtu aliye zaliwa na Mungu hatendi dhambi; bali yeye aliyezaliwa na Mungu hujirinda, wala Yule muovu hamgusi.1Yohana 5:18.

- **Nawapenda wengine kwa sababu namjua Mungu**

Kila apendaye amezaliwa na Mungu, naye amezaliwana Mungu.1 yohana 4:7

- **Ninaishi katika ushindi**.

Kwa maana kila kitu kilicho zaliwa na Mungu hushinda ulimwengu; na huku ndiko kushinda ulimwengu hiyo imani yetu 1Yohana 5:4.

- **Mimi ni kiumbe cha kiroho**.

Yesu alisema. Kilicho zaliwa na Roho ni roho. Yohana 3:16.

**<u>Sasa ninaishi katika eneo la kiungu lisilo la kawaida (waefeso 1)</u>**

- ✓ Baraka zote za rohoni. ndani ya Kristo (aya 3).
- ✓ Kwa damu Yake, tunao ukombozi wetu (aya7).
- ✓ Msamaha wa dhamb (i aya 7)
- ✓ Siri ya mapenzi yake (aya 9)
- ✓ Urithi usio wa kawaida (aya 11)
- ✓ Hekima, ufunuo usio wa kawaida katika kumjua yeye (aya 17).
- ✓ Washiriki wasio wa kawaida kwa sa babu tumeketishwa na Kristo katika ulimwengu war oho. Waefeso 2:6
- ✓ Nimepata njia ya kumkaribia Baba katika Roho mmoja. Waefeso 2:18

- **Niko huru kwa sababu nimezaliwa kulingana na roho**

Ndiposa, ndugu zangu, sisi si watoto wa mjakazi, bali tu watoto wa huyo aliye mungwana,
Gal 4:31

- **Nilifanyika mtoto wa mungu.**

Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu.Yohana 1:12.

Tayari tumeona yakwamba kuzaliwa mara ya pili yamaanisa tumezaliwa kutoka mbinguni. Nimezaliwa mara ya pili kwa sababu Mungu anatamanihaya …

Ambaye hutaka wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli. 2 Timotheo1:4.

Kwa kupenda kwake mwenyewe alituzaa sisi kwa neno la kweli, tuwe kama limbuko la viumbe vyake. Yakobo 1:18.

**Hivyo ni tumezalIwa kwa mapenzi ya Yohana1:13.**

# NIFANYE NINI NIZALIWE MARA YA PILI?

**SEHEMU YA [B]**

**1.**

Ninaliamini neno la
Yesu kristo.
Yohana 1:12

**2.**

Nimepokea Yesu
katika maisha yangu.

Hakuna kitu kinaweza kuharibu hari yangu ya kuzaliwa mara ya pili'uhusiano na Mungu kwa sababu msingi wake uko juu ya neno {Neno lisilohalibika} la Mungu ambalo nilakutegemewa kikamilifu, kwa imani nina pokea ahadi ya Mungu [Mbegu}na kumpokea Yesu {Mbegu}ndani ya mioyo yetu.

Nimezaliwa mara ya pili:si kwa mbegu ihalibikayo bali kwa isio halibika; kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo milele 1 Petro 1:23

Mungu alikuwa ameahidi mbegu hii na ushindi atakao upata, katika bustani ya eden.

Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke na kati ya uzao wako na uzao wake; huo utakuponda kichwa, na weweutaponda kisigino. Mwanzo 3:15

Kuzaliwa mara ya pili yamaanisha kwamba niipokee hii mbeguya ushindi {Yesu} ndaniya maisha yanguna niyaishi maisha yangu ndani ya ushindi ambao ameshinda dhambi na kifo.

**MTU ANAZALIWA MARA YA PILI NDANI YA INJILI.**

- Soma hadithi ya zakayo katika Luka 19:1-10.
- Zakayo alitafuta kumwona Yesu [aya3]
- Alionyesha toba kwa kuvirudisha vitu alivyokua ame wanyangaya watu{aya8]
- Yesu alitangaza kwamba imani alioonyesha Zakayo imeleta wokovu kwa nyumba yake. {aya9}.

Kuzaliwa mara ya pili lazima tuwe kama Zakayo:

- Kupenda kujua zaidi habari za Yesu.
- Kumpokea kwa shangwe mioyoni mwetu.
- Kuitikia neno lake kwa imani

**NINI HUFUATA BAADAYE?**

Yesu anasema mara tu tumeamini tunao uzima wa milele.

ili kila mtu amuaminiye asipotee mbali awe na uzima wa milele.
Yohana 3:16.

Yesu anasema kwamba hatuwezi kuuona ufalme wa mbinguni wala kuuingia tusipo zaliwa mara ya pili. Yohana 3:3, 5.
Alianza huduma yake na kutuambia tumbuni na kuamini, kwa kuwa ufalme wa Mungu umekaribia.

Tubuni na kuamini injili. Mariko 1:15.

**UBATIZO UNAFUATA - KUAMINI NA KUTUBU**.
Katika mwisho wa huduma yake Yesu alituambia jinsi ya kuingia katika ufalme wa Mungu. Aaminiye na kubatizwa ataokoka, Mariko 16:16

Katika siku ya pentekote, umati uliokusanyika ulishawashika kwa dhambi kwa Roho mtakatifu. Walilia wakauliza wafanye nini. Jawabu ya Petro ilkuwa kuwaambia ubatizo hufuata toba ya kweli.

Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina la yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi. Namtapokea kipwa cha Roho mtakatifu, Matendo 2:38.

Kuja kwa yesu na ubatizo zaambatana
Kutubu kuja kwa Kristo → **Ubatizo** → Kupokea kipawa cha Roho mtakatifu.

**Nimezaliwa mara ya pili kikamilifu na kunganishwa na kanisa la yesu kristo!**

**UFAHAMU WA UBATIZO WA MAJI**.

Yesu alibatizwa ili kutimiza haki yote. "Kubari hivi sasa ili; kwakua ndivyo ipasavyokutimiza haki yote", Mathayo 3:15

Mfano wake ni:

- KutuambiaMungu antarajia ubatizo.
- Nimaandalizi ya huduma ya umma

**TUNATAMBULISHWA NA KRISTO KUPITIA UBATIZO**.
Fudisho kutoka Warumi 6:3-10

v.3. Tunatambulishwa na mauti yake.
v.4. Tuna tambulishwa na kuzikwa kwake.
v.5. Tuna tambulishwa kwa mfano wa kifo chake, kwa mfano wa kufufuka kwake.
v.6. Utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye.
v.7. Tumehesabiwa haki na dhabi.
v.8. Tulikufa pamoja na Kristo, Tunaishi pamojai naye.
v.9. alishinda kifo. Aya
v.10. Alifia dhambi mara moja tu, Amwishia Mungu.

**Kupitia ubatizo tunazifia dhambina kuingia kikamilifu kwenye uzima na Kristo aliye fufuka.**

**KANISA LA KWANZA LILIKUWA NA WATU WALIOBATIZWA.**

Petro alikuwa amehubiri kwamba Yesu ndiye Bwana na masihi Kristo.Iingekuaaje wasikilizaji kuingia katika ufalme kwa kuwa walikuwa wamesherehekea kusulubiswa kwake?

**Petroalisema**:

Tubuni, mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhabi zenu, nanyi mtapokea Roho mtakatifu. Matendo 2:38

Matokeo kanisa lilikua.

Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu elfu tatu . Matendo 2:41

**KANISA LILIENEA**

1. Mtu kutoka kushi anasikia neno na kuuliza ubatizo wa maji. Huyu towashi aliandalika kwa huduma kabla arudi kwa mji wake.

Tazama, maji haya ni nini kinacho zuia nisibatizwe. Matendo 8:36

Kupitia ubatizo wa maji alitengwa kama kuhaniwa Munguna injiri ikafika Afrika. Masharti tu ya ubatizo huu ni kwamba amuamini Bwana Yesu kristo kama mwana wa Mungu.

Ukiamini kwa moyo wako wote. Matendo 8:37
.

Jawabu yake ilirithisha jawabumasharti ya ubatizo. “Naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye mwana wa Mungu”. Matendo 8:37

.

2. **Watu wa mataifa wanakubaliwa katika mwili wa kristo.** Matendo 10:44.
   Wakati Petro alihubiri katika nyumba ya kornelio Roho Mtakatifu aliwashukia wale wote waliolisikia neno.

Mataifa walijazwa na Roho mtakatifu na kuongea kwa ndimi. Wayahudi walioamini walistajabu.

Ninani awezaye kukataza maji, hawa wasibatizwe watu waliopokea Roho mtakatifu vile vile kama sisi. Matendo 10:47

Na Petro akaamrisha wabatizwe katika njina la Bwana, Matendo 10:48

.

Mataifa walioamini wakaongezeka kwa mwili wa Kristo.

## MARA TUNAPOZALIWA MARA YA PILI NA KUBATIZWA TUNAKUWA SEHEMU YA MWILI WA KRISTO NA MAISHA YETU MAPYA YANAAZA.

Sura Ya Pili

# NITAMUELEKEZAJE MTU MWINGINE KWA KRISTO?

- HAKIKISHO LA WOKOVU WANGU MWENYEWE

Ninaongea juu ya yale ninayo yajua.

- Ninamjua Yesu Kristo binafsi.
- Nina uhusiano wa karibu naye.
- Ninajua yale amenitendea.
- Ninatamani kuona watu wote wakiokolewa.
- Nina uwezo wa kuongea kwa uhuru na kwa msukumo juu ya Yesu.

Yesu aliuliza wanafunzi wake.

Nanyi mwaninena mimi kuwa nani?
Mathayo16:15.

Kabla ya kumuelekeza mwingine kwa Kristo lazima tujibu swali hili Yesu aliuliza wanafunzi Jawabu ya Petro ilimfurahisa yesu.

Wewe ndiwe Kristo, mwana wa Mungu aliye hai. Mathayo16:16.

Ilikuwa ni juu ya imani ambapo Petro alijieleza hapa –imani ijayo kama ufunuo kutoka kwa Mungu-abapo Yesu alisema atalijenga kanisa.

Mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni, nakuambia wewe ndiwe Petro na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda. Mathayo16:18.

Nikutokana na imani kama ya Petro. Hii ni, kumjua Yesu kwa njia hii itatuwezesha kuzungumza naye kwa uhakika. Na yesu ameahidi ya kwamba Roho atatusaidia.

Yesu alisema - Aniaminiye mimi, kama vile maadiko yalivyo nena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake, Yohana 7:38.
Kinacho toka ndani yetu –miyo yetu-kitaleta uzima kwa wengine.
Mtume Paulo aliweza kusema.

Kwa maana ninamjua Yule niliye muamini. 2 Timotheo 1:12.

Lengo letu ni kumtambulisha tunaye mjua kwa watu wengine.

Niyamuhimu piakueleza vyema yalealiyo tutendea Yesu. Huu ni ushuhuda wetu binafsi.

- Nilikuwa namna gani kabla ya kukutana naYesu na kumkubali kama mwokozi wangu?
- Nilikutana na Yesu aje?
- Ninini kilitendeka nilipokutana na yesu
- Yesu ameyabadilisha aje maisha yangu?

Hakuna mtu anaweza kunipokonya kile Yesu amenitendea. Ukitumia mwelekeo uliopewa, jifunze kuandika ushuhuda wako binafsi.

- UKRISTO NI IMANI ILIOFUNULIWA.

Kuwa na hakikisho ya wokovu wako, sasa una ujasiri kumuelekeza mwingine kwa kristo. katika hatua nyingine unaweza kuuliza: Je ungetaka kujua zaidi kuhusu Yesu?" kama mwingine akijibu kwa uhakika, Omba pamoja nao.

"Yesu ningependa kujua mengi kukuhusu, je utajithihirisha kwangu?"

Kwa maana Yesu ameahidi kujifunua kwa wale wanamtafuta kwa bidii, anafurahia kujibu ombi hili ,na tuna uhuru wa kumuelekeza mwingine kwa hatua za kumpokea Yesukama Bwana.

"Huwapa thawabu wale wamtafutao".
Waebrania 11:6.

## HATUA ZA KUMUELEKEZA MTU MWINGINE KWA KRISTO.

1. **Niyamuhimu atabue dhambi maishani mwake na umuhimu wa mwokozi.**

Kwa maana wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa mungu. Warumi 3:23.
Uhakikishiwe ya kwamba alikuja kutafuta kilicho potea.

Kwa kuwa mwana wa adamu alikuja kutafuta kile kilicho potea. Luka 19:10


Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe wa pekee, ili kila mtu Amuaniniye asipotee, bali awe na uzima wa milele Yohana 3:16

Jua ya kuwa hakuna hukumu kutoka kwa Mungu kwa wale walio mgeukia.

Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu ukolewe katika yeye Yohana 3:17

2. **Mgeukie Mungu na utubu dhambi**.

DHAMBI.



MUNGU

Ongeza ombi fupi la toba - "NASIKITIKA KWAMBA NIMEFANYA DHAMBI."

3. **Pokea Mesamaha kwa imani**

> Tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu na kutusafisha na uthalimu wote.1Yohana 1:9.

Kukiri, huku kwa dhambi zetu yatuelekeza kwa **<u>musamaha</u>** na **<u>Kuoshwa.</u>**

<u>Aibu yote na hukumu zashughulikiwa hapa</u>. Kuna kubadilishana msalabani tunapokiri dhambi zetu, Yesu asiye na dhambi, anatubadilishia haki yake. {Yeye ni mwenye haki mbele za Mungu kwa sababu hana dhambi} kwa dhabi zetu. Yeye huchukua dhambi zetu; tunapokea haki ya kusimama na Mungu.

Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yenu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika yeye (2 wakorintho 5:21).
Ongoza kwa ombi la shukrani na msamaha na kuoshwa – "<u>ASANTE YESU KWA KUFA KWA SABABU YANGU NA KUNISAMEHE</u>".

4. **Karibisha Yesu aje na awe Bwana wa maisha yako, kumkaribisha Roho mtakatifu aje aishi ndani yako.**

"Roho mtakatifu tafadhali joo na uishi ndani yangu. Ninakupa ruhusa kutawala maisha yangu".

| **POLE** | **ASANTE** | **TAFADHALI.** |
|---|---|---|

Mtu amezaliwa mara ya pili nayu tayari kubadilika. Tunajipatiana mapenzi yetu na Yesu haki ya kutamalaki ndani ya maisha yetu. Kujinyenyekesha na Yesu atawale.

**Kuamini** Inafuatwa na **Ubatizo**

Yesu alisema: "Basi, enedeni, mkawafanye mataifa wote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana na Roho mtakatifu, na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi, na tazama, mimi nipo pamoja nanyi hata utimilifu wa dahali, Mathayo 28:19.

Kuwafundisha waamini wapya juu ya ubatizo wa maji ni sehemu ya kumuelekeza mtu kwa Kristo. Nihatua ya kwanza ndani ya "kuwafundisha kuyasika yale yote niliyo waamulu"

*KWA KUZITUMIA HATUA HIZI NNE KAMA MFANO, FANYENI MAZOEZI WAWILI WAWILI JINSI YA KUMUELEKEZA MTU KWA KRISTO.*

Sura Ya Tatu

# YESU MTUMISHI WA MUNGU

- Kutimiza unabii.
- Yesu kufunza juu ya ukuu.
- Yesu mfano kwetu.

1. **KUTIMIZA UNABII.**

Yesu anatangaza wajibu wake kama mtumishi.

- Akasema kujihusu:

Kama vile mwana wa Adamu asivyo kuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake kuwa fidia ya wengi. Mathayo 20:28.

Lakini mimikwenu ni kama atumikaye. Luka 22:27.

Hii ilikuwa kutimiza unabii akasema kujihusu.

Musidhani ya kuwa nilikuja kutangua maandikoau manabii, la sikuja kutangua, bali kutimiza. Mathayo 5:17.

**YESU ALITIMIZA UNABII NA MUNGU AKAMTUKUZA**.

Mungu wa Ibrahim na wa Isaka na wa Yakobo, Mungu wa Baba zetu, amemtukuza mtumishi wake
Yesu ambaye ninyi mlimsaliti na kumkana mbele ya pilato, alipokuwa ametoa hukumu yake afunguliwe. Matendo 3:13

**AHADI YA KIUNABII YA MTUMISHI WA MUNGU**.

- Soma Isaya 42:1-4.

Yesu alitabiriwa kama Yule ampendezaye Mungu, ilitimizwa na Roho wa Mungu, na kuleta haki kwa mataifa.

Mungu anasema:

Tazama mtumishi wangu nimtegemezaye.
Mteule wangu, ambaye nafsi yangu imependezwa naye. aya1

.

Nimetia Roho yangu juu yake.aya 1
Atawatolea mataifa hukumu. aya.1

- Soma Isaya 49:5-6.

Mtumishi huyo atayainua makabila ya yakobo na kuwakusanya Israeli wamrudie Mungu. Ataleta nuru kwa mataifa.

Upate kuwa wokovu wangu hata miisho ya dunia. aya 6.

- Soma Isaya 50:10.

Mungu anayaita mataifa yamche Bwana na wamtii mtumishi wake.

Ninani miongoni mwenu amchae Bwana? aya 10

.

- Soma Isaya 52:13.

Aya hii yaogea juu ya mtumishi wa Mungu atakaye teseka kwa sababu ya dhabi za mwanadamu. Mungu amesema.

Tazama, mutumishi wangu kwa busara, atatukuzwa, na kuinuliwa juu, naye atakuwa juu sana. Isaya 52:13

Yesu alitimiza aya hii na Mungu akamtukuza:

- ✓ Huyu ni mwanagu, ninayependezwa naye. Mathayo 3:17
- ✓ Huyu ni mwanagu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye; msikieni yeye. Mat.17:5.

## 2. YESU ANAFUNDISHA KUHUSU UKUU

- Wanafunzi wake walipokua wakizungumza kuhusu ukuu, Yesu alisema:

Maana aliye mkubwa ni yupi? yeye akiteye chakulani, au yule atumikaye? siye Yule akiteye chakulani? lakini mimi kati yenu ni kama atumikaye. Luka 22:27
.

- Anatuambia ya kwamba kufanyika mkuu lazima uwe mtumishi:

Na mtu yeyote anayetaka kuwa wa kwanza kwenu na awe mtumwa wenu; kama vile mwana wa Adamu asivyokuja kutumikiwa bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi Mathayo 20:27-28.

## 3. YESU – MFANO KWETU.

Soma yohana 13:1-17 - Ambapo Yesu anawaosha wanafunzi wake miguu. Yesu alikuwa na usalama katika ufahamu ya kwamba yeye ni wa Mungu, Baba.

> Yesu, hali akijua ya kuwa Baba amempa vyote mkononi mwake, nay a kuwa alitoka kwa Mungu naye alikuwa anaenda kwa Mungu aya. 3.

Tukiwa na uhakika wa umilele wetu, kuwatumikia wengine sio vingumu.
Yesu alisema:

> Kwa kuwa nimewapa kielelezo; ili kama mimi nilivyo watendea, nanyi mtende vivyo. aya 15

> Amin, amin nawaambia ninyi mtumwa si mkuu kuliko bwana wake wala mtume si mkuu kuliko yeye aliye mpeleka. aya 16.

> Mkiyajua hayo, heri ninyi mkiyatenda, aya 17.

**YESU ANAFUNDISHA KWAMBA TUKIWATUMIKIA WENGINE TUNAMTUMIKIA.**
Soma Mathayo 25:31-46

Katika fumbo hii Yesu ana wakaribisha wale:

- ✓ Wamewashibisha wenye njaa na kiu.
- ✓ Walio wakaribisha wageni.
- ✓ Waliowavika walio uchi.
- ✓ Walio watembelea wagonjwa na waliokua kolokoloni.

Yesu anawaambia waliotenda hayoyakwamba:

> ….kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo mlinitendea mimi. aya 40.

Vivyo hivyo anaonya yakwamba ambao hawatendi mambo haya:

> Kadiri msivyo mtendea mmojawapo wa hao walio wadogo hamukunitendea mimi.aya 45
> Yakobo anatuambia:

| |
|---|
| Vivyo hivyo na imani, isipokua na matendo imekufa nafsini mwake. Yakobo 2:17. |

**WITO WETU NI KUMFUATA YESU.**

Yohana 12:26 - Mtu akinitumikia → naanifuate; → nami nilipo, ndipo na mtumishi wangu ata atakapokuwapo

| |
|---|
| Tena mtu akinitumikia mimi BabaYangu atamheshimu. |

***"Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu abayo ilikuwemo pia ndani ya Kristo Yesu; ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa na sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho bali alijifanya hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa na mfano wa mwanadamu, tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba."***

**Wafilipi 2:5-8.**

Sura Ya Nne

# KUTUMIKA KAMA KUHANI WA BWANA

- Ninamtumikia nani?
- Nitamtumikia Mungu namna gani?
- Kutumika kama kuhani.

## NINAMTUMIKIA NANI?

Yesu alisema :

"Imeandikwa mshujudie Bwana Mungu wako, umuabudu yeye peke yake. Luka 4:8

Mtume Paulo anatukumbusha:

Kwa kuwa wao wenyewe wanatangaza habari zetu, jinsi kulivyokua kuingia kwetu kwenu; na jinsi mlivyo **mugeukia** Mungu mkaziacha sanamu, ili kumtumikia Mungu aliye hai, wa kweli.1Wathesolonike1:9.

Katika Wakolosai 3:23 - Lolote mfanyalo, lifanyeni kwa moyo, kama kwa Bwana, wala si kwa wanadamu & Aya 24 - Mukijuwa yakuwa mtapokea kwa Bwana ujira wa ulithi. Mnana mtumikia Bwa Kristo.

Wala hapatakuwa na laana yoyote tena. Nakiti cha enzi cha Mungu na cha mwana kondoo kitakuwamu ndani yake. Nawatumwa wake watamtumikia.Ufunuo 22:3

## NINA MTUMIKIA MUNGU NAMNA GANI?

- **Bila uoga**
  Baba yake Yohana mbatizaji, Zacharia, alitabiri yakwamba lazima tumtumikie bila uoga. Luke1:74.

Alisema tutayatenda haya.

Kwa utakatifu na kwa haki mbele zake siku zetu zote. Luka 1:75.

Kwa maana tumewekwa huru kutoka dhabi.

- **Kwa dhamiri safi**

Damu ya yesu inanyunyiza moyo wangu na kunitakasa kutokana thamila mbovu. Waebrania 19:22.

Basi si zaidi damu yake Kristo, ambaye kwamba kwa Roho wa milele alijitoa nafsi yake iwe sadaka kwa Mungu kuwa sadaka isio na mawaa, itawasafisha dhamili zenu na matendo mafu, mpate kumwabudu Mungu aliye hai. Waebrania 9:14.

- **Katika upya wa roho.**

Mara tu alipozaliwa mara ya pili mtume Paulo, alitambua umuhimu wa kutumika ndani ya Roho

> *Bali sasa tumefunguliwa katika tolati, tumefia hali ile ilitupinga, ili sisi tupate kutumika katika* hali mpya ya roho, si katika hali ya zamani, ya adiko. Warumi 7:7.

- **Ninatumika na moyo wangu uliozaliwa mara ya pili.**
  Mtume Paulo anashuhudia:

> Kwa maana Mungu, nimuabuduye kwa roho yangu katika Injiri ya mwana wake, ni shahidi wangu jinsi niwatajavyo pasipo kukoma. Warumi 1:9.

- **Kwa kumheshimu na kumcha Mungu.**

> Basi kwa kuwa tunapokea ufalme usioweza kutetemeswa, na tuwe na neema, ambayo kwa hiyo tumtolee Mungu ibada ya kumpendeza, pamoja na unyenyekevu na kicho. Waebrania12:28.

- **Ninautoa mwili wangu kama thabihu iliyo hai.**

> Ndiyo ibada yenu yenye maana. Takatifu, ya kumpendeza Mungu, Warumi 12:1

Hii inahushisha "thabihu ya sifakwa Mungu, hii ni tunda la midomo yetu, tukirishukuru njina lake" Waebrania 13:15.

- **Bila-kukoma**

- Yohana anasema wale wanaokizunguka kiti cha enzi "Wanatumika mchana na usiku katika hekalu" Ufunuo7;15
- Ana katika Luka 2:37 hakutoka kwenye hekalu bali alimtumikia Mungu katika kufunga na maombi usiku na mchana.

**TWAMTUMIKIA MUNGU KAMA MAKUHANI.**

Mungu alimpa Musa mfano wa kujenga pahali patakatifu palipoitwa {hema ya makutano} ambapo makuhani walitumika mbele ya Mungu.pia akampa Musa mfano wa kufuatwa na makuhani kama kielekezo cha mambo yatakayo kuja. Katika mfano huu alioupatiana Mungu, makuhani walitakiwa kutoa thabihu za sifa, maombi, ibada.

> "Basi vitu hivi vikiisha kutengenezwa hivyo, makuhani huingia katika hema hiyoya kwanza daima, wakiyatimiza mambo ya ibada. Webrania 9:6

**LEO TUMEITWA TUWE MAKUHANI WA MUNGU ALIYE JUU.**

- **Kutoa sifa mbele ya Mungu wetu.**

> Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa mlki ya Mungu, mpate kutangaza fathili zake yeye aliye waita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu. 1Petro 2:9

.

- **Kuzitoa thabihu za rohoni**

> Ninyi nanyi kama mawe yaliyo hai, mmejengwa muwe nyumba ya Roho, ukuhani mtakatifu, mtoe dhabihu za roho, zinazokubaliwa na Mungu, kwa njia ya Yesu Kristo. 1 Petro2:5

**DHABIHU HIZI ZA KIROHO NIZIPI**?

- ✓ Maombi
- ✓ Sifa
- ✓ Kujipatiana Kusoma neno la Mungu
- ✓ Kuwaombea wagojwa
- ✓ Kujazwa na Roho mtakatifu
- ✓ Kulisikiliza neno la Mungu
- ✓ Kushirikiana katika kuumega mkate.

**<u>ZOEZI</u>**

1. Soma Warumi 12:1 kama kikundi kila mtu akiupatiana mwili wake kwa Bwana.

Tumia muda katika maombi ukizitoa sehemu za mwili wako ambazo zimeasi sana (kwa mfano mawazo yanayo poteza mwelekeo, ulimi unao potea njia, tamaa inayo tawala.}

2. Soma Warumi 13:15

Ukitumia maandiko yafuatayo na Zaburi za kuabudu, “toa dhabihu ya sifa kwa Mungu, tunda la midomo yetu, hiyo ni, kushukuru njina lake”

- ✓ Ufunuo 4:8
- ✓ Ufunuo 4:11
- ✓ Ufunuo 5:9-14
- ✓ Ufunuo 7:12
- ✓ Ufunuo 11:17
- ✓ Ufunuo 15:3-4
- ✓ Yuda 24-25
- ✓ 1Timotheo 6:15b-16

Himiza mwelekeo wa ibada kwa Mungu Baba, Yesu Kristo mwana, na Roho mtakatifu mbarikiwa.

Sura Ya Tano

# KUTUMIKIA MWILI WA KRISTO NA VIPAWA VYA ROHO MTAKATIFU

- Vipawa vya Roho mtakatifu
- Vipawa vya Bwana mfufuka
- Vipawa vya Mungu, Baba
- Kila mwamini akihudumu
- Tabia za mutumishi

***Basi pana tofauti za karama; bali Roho ni Yeye Yule.Tena pana tofauti za huduma, na Bwana ni yeye Yule.Kisha pana tofauti za kutenda kazi, bali Mungu ni yeye Yule azitendaye kazi zote katika wote.* 1Wakorintho 12:4-6**

Hizi vipawa vya Roho mtakatifu, Kristo mfufuka, na Mungu Baba zinapatianwa kanisani la Bwana Yesu, ili likuwe na kukamilika.

> Lakini kila mmoja hupewa ufunuo wa Rohokwa kufaidiana, 1 Wakoritho 12:7

<u>**VIPAWA VYA ROHO MTAKATIFU**</u> - "KUNA TUFAUTI ZA KARAMA LAKINI ROHO NI YEYE YULE."

Mtume Paulo anataka tujue, tuelewe na tutamani vipawa vya Roho.

> Basi kwa habari ya karama ya Roho, sitaki mkose kufahamu.1Wakorintho 12:1

> …kutaka sana karama za rohoni.1Wakorintho 14:1

Karama za rohoni zinaelezwa katika 1Wakorintho 12:8-10

- **Vipawa vya ufunuo -** Mungu hufunua maarifa yake kwetu kupitia:

NENO LA HEKIMA | NENO LA MAARIFA | KUPAMBANUA ROHO

- **Karama za kuthihirisha -** Mungu huthihirisha nguvu zake kwetu kupitia:

MATENDO YA MIUJIZA | KARAMA ZAKUPONYA | IMANI

- **Karama za mawasiliano** - Mungu huwasiliana nasi kupitia

| AINA ZA LUGHA | UNABII | TAFSIRI YA LUGHA |
|---|---|---|

**Hizi karama za roho ni za kufaidi mwili wote.**

- Zinaelekeza katika mikutano ya maombi Mungu anapo wasiliana kupitia kalama ya unabii.
- ZInamuelekeza mshauri katika ushauri wa maombi Mungu anapo thihilisha neno la maarifa na neno la hekima na kumwezesha mshauri kubabanua hiyo roho.
- Zinathihilisha nguvu za Mungu kupitia uponyaji, miujiza, na kuachilia imani katika nguvu za Mungu.

Lakini kazi hizi zote anazitenda Roho huyo mmoja, akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye.1 Wakorintho12:11

## VIPAWA VYA BWANA MFUFUKA

"Pana tofauti ya huduma, bali Bwana ni yule mmoja"

Waefeso 4:11: Kristo mfufuka ametoa kwa kanisa

| **mitume** | **manabii** | **wainjilisti** | **wachungaji** | **waalimu** |
|---|---|---|---|---|

Wale waliochaguliwa na Bwana katika ofisi hizi wanapotumikia mwili wa Kristo, tunaona:

- Watakatifu wakikamilishwa
- Huduma zinainuka
- Mwili wa Kristo unahimizwa na kujengeka [Waefeso 4:12]

Mtume na Nabii wanaweka msingi [Waefeso 2:20] ambapo huduma zingine zinajenga.

- Mitume wanaongea mafundisho ya Bwana wakileta ufunuo wa mapenzi ya Bwana katika mwili wa Yesu.
- Nabii anaongea neno la Bwana akilielekeza kanisa.
- Mwinjilisti anendainje akihubiri injili ya Yesu na kuwaleta waamini wapya kanisani.
- Muchungaji anawalea waamini wapya.
- Mwalimu ana waelekeza waamini wapya ndani ya neno la Mungu.

## VIPAWA ZA MUNGU, BABA

"Kuna shughuli tofauti, bali ni Mungu Yule atendaye kazi yote ndani ya yote"

Soma Warumi 12:3-8

Mungu alipatiana zawadi hizi alipotuumba. Hii inamaanisha kila mmoja katika mwili wa yesu ana moja ya zawadi hizi au zaidi katika maisha yao.Kwa maana ni zawadi za neema kila mshiriki wa mwili wa Kristo anaweza kuita mojowapo ya zawadi hizi kama inavyohitajika.

Aya 6. Tuna zawadi zilizo mbalimbali kwa kadili ya neema tuliyopewa

| ZAWADI HIZI NI ZIPI? | TUNAZITUMIA NAMNA GANI? |
|---|---|
| **Aya.6. Unabii** | **kwa kadiri ya imani.** |
| **Aya.7. Huduma** | **katika kuhudumu.** |
| **Aya.7. Kufundisha** | **katika kufundisha kwake.** |
| **Aya.8. Kuhimiza** | **katika kuhimiza kwake.** |
| **Aya.8. Kutoa toa** | **kwa ukarimu** |
| **Aya.8, Kusimamia** | **kwa bidii.** |
| **Aya.8. Kurehemu** | **kwafuraha.** |

**Zote tumepewa zawadi tofauti kwa maana kanisa ni mwili wa Kristo na kila mshiuriki ana sehemuya mhimu katika utendaji kazi wamwili huu.**

"Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila kimoja peke yake.1 Wak.12;27

**MUNGU AMEYAWEKA MAJUKUMU KANISANI**

Namungu ameweka wengine katika kanisa, wa kwanza mitume, pili manabii, tatu waalimu, kisha miujiza, karama za kuponya wagonjwa na masaidiano, na maongozi na aina ya lugha.1Wakorintho 12:28.

JE, SISI SOTE TUNA KALAMA HIZI? HAPANA! HATAHIVYO, ZIPO NDANI YA MWILI WA KRISTO. HIVYO ZINA WASHIRIKI FURANI WA KANISA ILI WOTE WAPOKEE FAIDA YAZO.

- ➔ Takeni sana karama zilizo kuu 1wakorintho12:31

**KILA MUAMINI ANAHUDUMU**

- **Katika upendo**

Maana ninyi, ndugu, mliitwa mpate uhuru; lakini uhuru wenu usiwe sababu ya kuufuata mwili, bali tumikianeni kwa upendo. Wagaratia 5:13

Yesu alitufundisha ya kuwa amri kumuni kupendana-Mungu kwanza, tena jirani. Luka 10:27

Tusiwe kwazo la namna yo yote katika jambo lolote, ili utumishi wetu usilaumiwe.2 Wakorintho 6

- **Kwa zawadi za kiroho**

Mtume Paulo hataki tusizielewe vipawa vya kiroho. Anatuambia tutamani kalama zaikiroho.

Ufuatene upendo, na kutaka kalama za kiroho.1Wakorintho 14:1

> Basi pana tofauti za zawadi; bali Roho ni yeye Yule.1Wakorintho 12:4

Pia anatukubisha ya kwamba bila upendo twaweza kuwa na zawadi nyingi na tusifaulukati huduma.

> Nijapo sema kwa lugha za wanadamu na za maraika, kama sina upendo, nimekuwa shaba iliyo na upatu uvumao.1Wakoritho 13:1

- **Kwa karama za neema**

**[a]** Kutoka kwa Mungu Baba

Katika kuumba, Mungu amempa kila mtu zawadi ambazo zinatusukuma, ili tutende, na ametupa neema ambayo inatuwezeshakuzitumia karama hizi ku jenga wengine walio washiriki wa mwili wa Kristo kila mshiriki lazima atumie karama hizi kuwatumikia wengine, na wengine katika mwili wa Kristo wanafaidika wakati kila mshiriki anatumika. Hizi ni karama za Mungu.kwa kiai mtu, Anaweza kutarajia kupokea. awe na moja yapo ya zawadi hizi.

> Kwa kuwa kama vile katika mwili mmoja tuna viungo vingi, wala viungo vyote havitendi kazi moja, vivyo hivyo sisi tulio wengi tu mwili mmoja katika Kristo, na viungo, kila mmoja kwa mwenzake. Warumi.12:4-5

Katika kufundisha juu ya kalama hizi, mtume Paulo anatuhimiza: hebu tuzitumie.

**[b]** Kutoka kwa Bwana Bwana mfufuka

Mara tu tunapo zaliwa mara ya pili, tunapewa neema ambayo inatuwezesha kupokea ufunuo wa kiutumekatika mwili wa Kristo.Upako wa Bwana unaleta ufunuo. Msingi wa kimaandiko juu ya maisha yetu unawekwa kulingana na neno la Mungu na tunakuja katika ukomavu. Kwa njia hiyo hiyo kanisa linapokea ufunuo na kukua. Ufunuo wa kiutume una weza kupokelewa na yeyote.

SOMA: Waefeso 4:13-16

Matokeo ya kiutume ni yapi?

- ✓ Sote tunaufikia umoja wa imani
- ✓ Nakumfahamu mwana wa Mungu
- ✓ Kuwa mtu mkamilifu
- ✓ Kufikia kwenye cheo cha kimo cha utimilifuwa Kristo
- ✓ Tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa hukuna huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu.
- ✓ Kwa hila ya watu, kwa ujaja, tukizifuata njia za udanganyifu.
- ✓ Lakini tushike kweli katika upendo.
- ✓ Na kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo.

Kakika njia hiyo, kila muamini anaweza kusikia <u>sauti ya kiunabii ya Mung</u> una kukua .Mungu anaendelea kunena na kanisa lake.Yeye anapatiana ndoto na maono vile vile kutuzungumzia kupitia neno la Mungu.kila kiungo katika mwili chaweza kusikia sauti ya Mungu ikileta ushawishi wa dhabi na muelekeo wa toba.

Yesu ameahidi kulinjenga kanisa lake {Mathayo 16:18}, kwa hivyo twaweza kutalajia yeye kutuelekeza.

Kila muamini aliyezaliwa mara ya pili amehisi neema ya wokovu ya Bwana Yesu Kristo. Kwa hivyo kila muamini ana ushuhuda wa yesu wa kushiriki na mtu mwingine.kwa hivyo kila mmoja anaweza <u>kufanya kazi ya uinjilisti</u> kama anavyo elekezwa na Mungu.

Zote twaweza kuwa wachungajikwa mtu mwingine. Mchungaji anashughulikia watu wengine. Mala tu tunapozaliwa mala ya pili, "upendo wa Bwana umemwagwa ndani ya mioyo yetukwa Roho mtakatifu tulie patiwa" [Warumi 5:5], na sio vingumu kuvutwa kwa mtu mwingine kwa njia ya kumshughulikia katika njia ya upendo.

Tunapokaribia kwa njia hiyo, tuna fulsa nyingi za <u>kufundisha kile tumejifunza juu ya Mungu</u>. Kwa hivyo kila mwamini anahudumu kama vile neema ya mungu inamuwezesha, na kila muamini ana fulsa ya kuja kwa ushawishi wa wale walio chaguliwa na Mungu katika ofisi ya: mtume, nabii, mwinjilisti, mchungaji, na mwalimu.

Matokeo ni kwamba kanisa lita:

> Kuwa hata kumfikia yeye katika yote, yeye aliye kichwa Kristo.katika yeye mwili wote ukiungmanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadili ya utendaji wa Kila sehemu, moja, huukuza mwili wote upate kujinjenga wenyewe katika upendo. Waefeso 4:15-16.

**TABIA ZA MTUMISHI**
Tabia zawalio itwa watumike ni zipi?

> Basi ndugu, chagueni watu saba miongoni mwenu, walioshuhudiwa kuwa wema,
> Wenye kujawa na Roho na hekima, ili tuwaweke juu ya jambo hili. Matendo: 6:3.

Hivi ndivyo yatupasa kuwa. Ni Roho mtakatifu hutuwezesha kukua, kuishi na kutembea ndani ya kalama zote za Mungu Baba, Yesu aliye fufuka na Roho mtakatifu ameweka ndani yetu, ili tuwe watu:

- Walioshuhudiwa kuwa wema.
- Wenye kujawa na Roho.
- Wenye hekima.
- Watu kama wao walichaguliwa "kutumika "katika kanisa la mwanzo matendo 6:2

<u>**ZOEZI**</u>.

- Kutoka warumi 12:6-8 orodhesha zawadi ambazo unajua Mungu amekupa.
- Tazama 1wakorintho 12;8-10

Kwa kikundi kidogo, muwekanie mkono na kuuliza Bwana aachilie vipawa kwa kila mtu. Ombea shauku iongezeke ya kumtumikia Bwana kwa kalama za Roho.

Sura Ya Sita

# YULE MTUMISHI MWOMBEAJI

- Kwa nini tuombe?
- Kuwaombea wale wanahubiri na kufundisa neno.
- Waombee watakatifu.
- Ombea watu wote.
- Nini kina tendeka na maombi ya watakatifu?

## KWA NINI TUOMBE?

Mtume Paulo anawahimiza waamini kuomba. "Dumuni sana katika kuomba, mkikesha katika kuomba na kusali. Wakolosai 4:2.

- ➢ Soma wakolosai 4:11-12

Paulo anampongeza Epafra, mtenda kazi pamoja name kwa ajili ya ufalme wa Mungu. {aya 11}

Epafra ni nani? | Ni mtumwa wa Yesu Kristo

Paulo anampongeza kwa nini? | Epafra …akifanya bidii sikuzote kwa ajiri yenu katika maobi.

Nikwanini Epafra anafanya bidii siku zote kwa waamini katika maombi?

> Ili kwamba msimame wakamilifu na kuthibitika sana katika mapenzi yote ya Mungu.

Bwana yesu Kristo anakuja kwa kanisa "…Kanisa tukufu ,lisilo na ila wala kunyanzi wala lolote kama hiyo;bali iwe takatifu isio na mawaa.Waefeso 5:27.

Sisi kama, Epafra, tuwe na "juhudi kubwa kwa watakatifu wote" {aya 13} "tukifanya bidii katika maombi" {aya 12} tutawaona watakatifu wamesimama wakamilifu na wakiwa wamethibitika katika mapenzi yote ya Mungu {aya12}.

Watakatifu ni akina nani? 1 wakorintho1:2 Walewaliotakaswa katika Kristo Yesu walioitwa wawe watakatifu. Pamoja na wote wanao liitia jina la Bwana wetu Yesu Kristo Bwana wetu.

> Lakini mwisho wa mambo yote umekaribia; basi; iweni na akili, mkeshe katika sala.1 petro.4:7

## KUWAOMBEA WATAKATIFU

- ➢ Soma waefeso 6:18-20

Mtume Paulo anatuhimiza kuomba bila kukoma kwa"

- ✓ Watakatifu wote
- ✓ Wale wanao hubiri neno la Bwana

Twaombeaje watakatifu wote?

> ✓ Kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote {aya 18}

**KUWAOMBEA WAHUBIRI NA WALIMU WA NENO**

Twawaombeaje wale wana hubiri na kufudisha neno?

> Pia na kwa ajili yangu mimi, nipewe usemi kwa kufumbua kinyuachangu, ili ni nihubiri kwa bidii ile siri ya injili (aya 19)

> Ambayo kwa ajiri yake mimi ni mjumbe katika minyororo; hata nipate ujasiri katika hiyo kunena jinsi inipasavyo kunena (aya 20)

**KUWAOMBEA WATU WOTE**

Soma 1 Timotheo 2:1-3 - Mtume Paulo anatuhimiza, kuwaombea watu wote kila mahali. Yatupasa kufanya:

Dua | Sala | Maombezi | Shukrani

kwa:

Watu wote | Wafalme | Wote wenye mamlaka.

**NI KWANINI TUWAOMBEE WENGINE?**

Hili ni nzuri nay a kukubalika mbele ya Mungu, Baba yetu aya. 3.

Ambaye hutaka watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli.(aya 4)

Tuishi maisha ya utulivu na amani, katika utauwa wote na ustahivu. (aya 2)
Yesu aliwaonya wanafunzi wake.

Yesu anawaonya wanafunzi wake:

Kesheni, mwombe, msije mkaingia majaribuni; Mathayo 26:41

Kanisa ambalo haliombi ni la kuhurumiwa na halina matunda.

**NININI KINATENDEKA KWA MAOMBI YA WATAKATIFU?**

- Soma Ufunuo 5:8

Maombi ya watakatifu yako namna gani? | Kama vitasa vya thahabu vilivyo jaa manukato |

- Soma Ufunuo 8:3-4

Ninini kinatendeka na maombi ya watakatifu? Yanapaa mbele ya Mungu kutoka mkono wa malaika

**ZOEZI:**

Katika vikundi vidogo ombeni mkizitumia aya hizi.

(A)Waamini wote.
Waefeso 1:15-19 Wakolosai 1:9-14 Wafilipi 1:3-6

(B) Kwa wale wanaohubiri na kufundisha neno la Mungu.
Waefeso 6:19-20 2Wathesolonike 1:11-12 Wakolosai 4:2-4

(C) Andika orodha ya watu unaowajua na hawaja okoka na uwaombee kwa majina.

(D) Waombee wenye mamlaka katika wilaya yako, mji, jiji, serekali….